# Notisi ya DSHS ya Shughuli za Faragha ya Taarifa za Matibabu ya Mteja

**DSHS Notice of Privacy Practices for Client Medical Information**

**Inatumika kuanzia Septemba 23, 2013**

DSHS lazima itakuarifu kuhusu haki zako za faragha za Sheria ya Ushuru wa Huduma ya Taarifa ya Afya na Kuwajibika (HIPAA). (45 CFR 164.520). DSHS ni "chombo mseto." Sio huduma zote za DSHS hutolewa na HIPAA, ni programu tu zilizoorodheshwa kama Vipengele vya Huduma ya Afya kwenye tovuti ya DSHS ndio hutolewa na HIPAA. Notisi hii inawahusu tu wateja wanaohudumiwa na programu hizo zinazotolewa. Notisi hii haiathiri ustahiki wako wa huduma za DSHS.

**Notisi hii inaeleza jinsi gani taarifa za matibabu kuhusu wewe zinaweza kutumika na kufichuliwa na jinsi gani unaweza kupata taarifa hizi. Tafadhali soma kwa umakini.**

**Ni nini PHI?**

Taarifa za Afya Zinazolindwa (PHI) ni taarifa za matibabu za mteja zinazohifadhiwa na pande za DSHS zitolewazo na HIPAA. PHI ni taarifa za matibabu zinazokuhusu wewe kuhusu hali yako ya kiafya au siha, huduma ya afya unayopata, au malipo kwa ajili ya huduma yako ya afya. DSHS inapaswa kulinda PHI yako kwa mujibu wa sheria.

**Nini PHI inafanya kuhusu DSHS ilichonacho kuhusu mimi?**

Kwa kutusaidia kukuhudumia, utahitaji kutupa taarifa za matibabu au afya pamoja na eneo lako, taarifa za kifedha na kumbukumbu za matibabu. Pia tunaweza kupata PHI kuhusu wewe kutoka vyanzo vingine vilivyohitaji kukuhudumia au kukulipia huduma yako ya afya.

**Nani anaona PHI yangu?**

Tunaona kiwangu kidogo sana cha PHI tunachohitaji ili kufanya kazi zetu. Huenda tukashirikiana PHI na programu nyingine au watu ikiruhusiwa na sheria au ukiidhinisha wewe. Kwa mfano, PHI yako inaweza kutolewa au kutumika na Mamlaka ya Huduma ya Afya na watoa huduma ya afya wengine ili kuratibu na kulipa huduma ya afya. Huenda tunashirikiana PHI ya zamani, ya sasa, au ya siku za mbele.

**Nini PHI inafanya kinachotolewa na DSHS?**

Tunashirikiana tu PHI yako ambayo watu wengine wanaihitaji kufanya kazi zao na kama ilivyoruhusiwa na sheria. Unaweza kuomba orodha ya watu ambao wameona PHI yako kwa malengo flani.

**Wakati gani DSHS hushirikiana PHI?**

Tunashirikiana PHI wakati wa "mahitaji ya kujua misingi" ili kuratibu huduma na kwa ajili ya tiba, malipo, na utendaji wa huduma ya afya. Kwa mfano, tunaweza kushirikiana taarifa ili kuamua ikiwa:

- Tiba ya matibabu inapaswa kutolewa.
- Tunaweza kulipa huduma kwa watoa huduma za afya.
- Unastahiki programu za DSHS.
- Huduma unayopata kutoka kwa watoa huduma inatimiza masharti ya kisheria.

**Je, naweza kuona PHI yangu?**

Unaweza kuona PHI yako. Ikiwa utaomba, utapata nakala ya PHI yako. DSHS inaweza kukulipisha kwa ajili ya nakala.

**Je, naweza kubadilisha PHI yangu?**

Ikiwa unadhani kwamba PHI yako ina makosa, unaweza kutuomba kuibadilisha au kuongeza PHI mpya. Unaweza pia kuomba tutume mabadiliko yoyote kwa wengine ambao wana nakala za PHI yako.

**Je, itakuaje ikiwa mtu mwengine anahitaji PHI yangu?**

Unaweza kutakiwa usaini fomu ili kuturuhusu kutoa PHI yako ikiwa:

- Tunahitaji idhini yako ili kutoa huduma au matunzo;
- Unatutaka tutume PHI yako kwa wakala mwengine au mtoa huduma kwa sababu zisizoruhusiwa na sheria bila ya idhini yako;
- Unataka PHI itumwe kwa mtu mwengine, kama vile wakili wako, ndugu au mwakilishi mwengine.

Idhini yako ya kushirikiana PHI yako ni nzuri mpaka tarehe ya mwisho unayoiweka kwenye fomu. Tunaweza tu kushirikiana PHI unayoirodhesha. Unaweza kughairi au kubadilisha idhini hii kwa kuwaandikia DSHS.

**Notisi ya DSHS ya Shughuli za Faragha kwa ajili ya Taarifa za Matibabu ya Mteja**
Inatumika kuanzia Septemba 23, 2013

| | |
|---|---|
| **Je, DSHS inaweza kushirikiana PHI yangu bila ya idhini yangu?** | DSHS inaweza kushirikiana PHI bila ya idhini yako katika baadhi ya matukio. Kisheria, tunaweza, kutakiwa au ruhusiwa kutoa PHI yako. Baadhi ya mifano ni pamoja na mahitaji ya:<br>• Kuripoti matukio ya unyanyasaji wa mtoto au mtu mzima au utelekezaji kwa Huduma za Uinzi wa Mtoto, polisi au wakala nyingine.<br>• Kutoa kumbukumbu chini ya agizo la mahakama.<br>• Kutoa PHI kwa wakala nyingine ambazo hukagua uendeshaji wa DSHS.<br>• Kushirikiana PHI na wakala nyingine ambazo hutoa leseni na kuchunguza vituo vya afya, kama vile nyumba za uuguzi na hospitali.<br>• Kushirikiana PHI na watoa huduma au wakala nyingine ili kukuhudumia wewe au kama itakavyohitajika ili kuamua kama unastahiki huduma au ruzuku.<br>• Kutoa PHI kwa walezi au wazazi wa watoto wadogo.<br>• Kutumia PHI kwa ajili ya utafiti.<br>• Kutumia au kufichua PHI katika hali ya dharura au kwa malengo ya misaada ya maafa. |
| **Je, naweza kuweka mipaka ya kushirikiana PHI yangu na jinsi gani naweza kuipata?** | Unaweza kutuomba tuweka mpaka wa matumizi na kushirikiana kwa PHI yako lakini sio lazima tukubaliane. Unaweza pia kutuomba tukutumie PHI yako katika umbile tofauti au eneo tofauti. |
| **Ni nini uvunjaji?** | Uvunjaji ni matumizi au ufichuaji wa PHI yako ambao haukuidhinishwa chini ya HIPAA, ikiwa ni pamoja na kupotea kwa kuibiwa, makosa au kudukuliwa. Tutakujulisha kwa barua ikiwa kuna uvunjaji wa PHI yako chini ya HIPAA. |
| **Je, naweza kupata nakala ya notisi hii?** | Ndio. Notisi hii ni yako ya kuhifadhi. Ikiwa umepata notisi hii kwa njia pepe ya mtandao, unaweza kuomba nakala ya karatasi na tutakupa nakala moja. |
| **Je, itakuaje ikiwa shughuli za faragha za PHI zitabadilika?** | Tunatakiwa kutii notisi hii. Tuna haki ya kubadilisha notisi hii. Ikiwa sheria au shughuli zetu za faragha zitabadilika, tutakutumia taarifa kuhusu notisi mpya na wapi utaipata au tutakutumia. |
| **Nani wa kuwasiliana nae ikiwa nina maswali kuhusu notisi hii au haki zangu za PHI?** | Ikiwa una maswali yoyote kuhusu notisi hii, unaweza kuwasiliana na Afisa Faragha wa DSHS kwa DSHSPrivacyOfficer@dshs.wa.gov au (360) 902-8278. |
| **Jinsi gani naweza kuripoti uingiliaji wa haki zangu za faragha za PHI?** | Ikiwa una amini kwamba haki zako za faragha za PHI zimeingiliwa unaweza kutuma malalamiko kwa:<br><br>DSHS Privacy Officer, Department of Social and Health Services, PO Box 45115, Olympia WA 98504-5115 au kwa barua pepe kwa DSHSPrivacyOfficer@dshs.wa.gov. Ikiwa utatuma malalamiko, DSHS haitabadilisha au kusimamisha huduma zako na haipaswi kukulipizia kisasi dhidi yako.<br><br>**AU**<br><br>Tuma malalamiko yako mtandaoni katika: https://ocrportal.hhs.gov/ocr/cp/complaint_frontpage.jsf au kwa kuandika kwa: Office for Civil Rights, US Department of Health and Human Services, 200 Independence Avenue, S.W., Room 509F HHH Bldg., Washington, D.C. 20201, phone (800) 368-1019. Malalamiko yoyote kwa DHHS lazima yafanyike ndani ya siku 180 za uingiliaji wa faragha unaodaiwa. |